**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI KITAMA**
**S.L.P 83**
**TANDAHIMBA.**
**19. 04. 2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**

**_________________________**

**S.L.P ____________________**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KITAMA HALMASHAURI YA WILAYA TANDAHIMBA MKOA MTWARA MWAKA 2024.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga Kidato cha tano katika Shule ya sekondari KITAMA iliyopo katika halmashauri ya wilaya ya TANDAHIMBA na atasoma tahasusi ya EGM.

Shule ya Sekondari Kitama ipo umbali wa Kilometa 18 upande wa Mashariki mwa makao makuu ya halmashauri ya wilaya Tandahimba.

Jinsi ya kufika shuleni, kuna njia mbili.

a. Kama unatokea Mtwara mjini kwa kutumia usafiri wa umma kuelekea Tandahimba shuka kituo kinachoitwa TANKINI ( pacha ya shule ya sekondari Kitama).
b. Kama unatokea kituo cha mabasi Tandahimba, tumia usafiri wa umma mpaka kwenye kituo kinachoitwa TANKINI ( pacha ya shule ya sekondari Kitama).

Muhula wa Masomo unaanza tarehe.......... hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe .............. Mwisho wa kuripoti ni tarehe.............**.**

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-**

**Sare za Shule**

i. Sketi mbili ndefu zinazoishia kwenye kifundo cha mguu (Rangi ni **Prussian blue)** mshono ni-rinda box mbele na nyuma mwanafunzi aje nazo. Kwa mzazi atakayepend***a,*** zitapatikana shuleni, ***s***keti Moja TSH 35,000/=, sketi 2 ni tsh 70,000/=.

ii. Mashati mawili (Tetron) rangi nyeupe mikono mifupi kwa wasiovaa hijabu na mikono mirefu kwa wanaovaa hijabu.

iii. Rangi ya Hijab ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

iv. Sare ya Michezo ni Track suti yenye rangi ya **dark blue** na raba nyeupe.

v. Sweta rangi ya( **prusssian blue 003151)** kwa ajili ya kujikinga na baridi.

vi. Magauni mawili ya kazi rangi ya **kijivu (grey)** mshono wa solo na yasiwe ya kubana.

vii. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.

viii.Soksi nyeupe za kutosha kwa mahitaji ya mwanafunzi.

ix.T-shirt rangi ya njano ya dhahabu(golden yellow), mwanafunzi aje nayo. Kwa mzazi atakayependa, zitapatikana shuleni kwa tsh 15,000/=

x.Taulo za kike za kutosha.

xi.Kanga doti moja.

xii.Shuka za pink jozi 2,foronya ya godoro 1, chandarua 1.

xiii. Godoro

Xiv.Nguo za ndani za kutosha

**2.1 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:**

i. Daftari(counter book 12 na faili mbili 2)

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika

iv. Scientific Calculator;

v. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

vi. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko na dumu la lita 5

vii. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.

viii. Kadi ya mfuko wa matibabu

ix. Sanduku imara la kuwekea vitu na kufuli lake

**NB: Mwanafunzi anashauriwa kuwa na vitabu vya masomo yake yote (General studies, Economics, Geography & Advanced Mathematics).**

**Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5000/= |
| 3 | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| 4 | Nembo | 5000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Michango hiyo ilipwe kwenye **akaunti namba 71001100009 NMB**

**Jina la akaunti: Maendeleo Kitama Sekondari**

**ZINGATIA: GHARAMA ZA MATIBABU NI ZA MZAZI.**

## 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari.
xi. Wizi ni utovu wa nidhamu,
xii. Kugoma na kuhamasisha migomo ni kosa.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2. Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
Viii.Uvutaji wa sigara;
ix.Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x.Kupata ujauzito au kutoa mimba
Xi.Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele
Xii.Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
Xiii.Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv.Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
Xv.Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi.Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii.Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4**. **VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU**

i. Fomu ya uchunguzi wa afya (medical examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali
ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni na maelezo mengine yanayotolewa na shule.
Iv.Picha nne(4) za wazazi na ndugu wa karibu wa wanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu

Kwa Niaba ya wanafunzi, walimu na wafanyakazi wote hapa shuleni **TUNAKUKARIBIBISHA SANA KITAMA SEKONDARI.**

**AHSANTE.**

**....................................**

**CONSOLATA C. NCHIMBI**

**MKUU WA SHULE.**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:**

- **Mkuu Wa Shule 0657 126 461**
- **Makamu Mkuu Wa Shule 0713 204 978**
- **Mwalimu wa Taaluma 0769 527 722**
- **Mwalimu Wa Malezi 0762 934 307**

**MKATABA WA KUTOSHIRIKI MIGOMO NA FUJO/VURUGU**

**(Fomu hii ijazwe na kurudishwa shuleni)**

Mimi ________________________________ ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha _____________katika shule hii, naahidi kutojihusisha kwa namna yoyote katika migomo, fujo au kosa lolote la Jinai ambalo litahatarisha

Amani au litakalokuwa kinyume cha Sheria, Kanuni na taratibu za shule.

Endapo ikithibitika kuwa nimetenda kosa au makosa tajwa hapo juu sitakuwa na pingamizi juu ya hatua za kinidhamu zitakazochukuliwa dhidi yangu.

Jina la mwanafunzi _____________________________________________

Sahihi ya Mwanafunzi ___________________________________________

Tarehe _________________________________

Jina la Mzazi/Mlezi ______________________________________________

Sahihi ya Mzazi/Mlezi ____________________________________________

Tarehe _________________________________

Anuani ______________________________
______________________________
______________________________
**Tarehe** ______________________

Mkuu wa Shule,
Shule ya sekondari kitama
S.L.P. 83
**TANDAHIMBA**

**YAH: BARUA YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE.**

Ahsante kwa barua yako **Kumb.Na** ______________________ya tarehe ____________

(a) Nakubali/ Sikubali nafasi niliyopewa ya kidato cha tano mwaka _________________
(b) Niko tayari/ siko tayari kufuata Sheria. Maagizo na masharti yote ya Kitama Sekondari
(c) Nitahudhuria/sitahudhuria masomo yote ninayotakiwa kusoma hapa shuleni
(d) Nikishindwa kuhudhuria bila sababu ya msingi nifukuzwe shule
(e) Nitaleta/sitaleta
    (i) Uthibitisho wa Uraia/Cheti cha kuzaliwa
    (ii) Vitu vinavyohitajika kwa matumizi yangu
    (iii) Cheti cha Afya

________________________________ ________________________________

**JINA NA SAHIHI YA MWANAFUNZI** **JINA NA SAHIHI YA MZAZI**

**TAARIFA BINAFSI KUHUSU MWANAFUNZI.**
**(Fomu hii ijazwe na Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi na kuleta shuleni)**

1. Jina la Mwanafunzi ______________________________________________
2. Kabila la Mwanafunzi ____________________________________________
3. (a) Wilaya aliyozaliwa Mwanafunzi ________________________________
   (b) Mkoa _______________________________________________________
4. Dini ya Mwanafunzi ______________________________________________
5. Tatizo la mwanafunzi kiafya
   _____________________________________________________________
   _____________________________________________________________
6. Tatizo la Mwanafunzi Kitabia
   _____________________________________________________________
   _____________________________________________________________
7. Jina Kamili la Baba Mzazi _________________________________________
   Anuani kamili __________________________________________________
   Kazi yake _____________________________________________________
8. Jina kamili la mama mzazi _________________________________________
   Anuani kamili __________________________________________________
   Kazi yake _____________________________________________________
9. Jina na Anuani kamili ya mtu/mlezi anayehudumia mahitaji muhimu ya mwanafunzi kama ada na vitu vingine
   _____________________________________________________________
   _____________________________________________________________
10. Uhusiano wa mwanafunzi na Mlezi ___________________________________
    Kazi yake _____________________________________________________
11. Orodha ya ndugu aliozaliwa nao mwanafunzi wakianzia na wa kwanza kuzaliwa. (Kama anasoma ataje darasa na shule.)

| Na. | JINA KAMILI | UMRI | KAZI | ANUANI YAKE |
|---|---|---|---|---|
| 01 | | | | |
| 02 | | | | |
| 03 | | | | |
| 04 | | | | |
| 05 | | | | |
| 06 | | | | |

12. Baba na mama wa Mwanafunzi wanaishi pamoja, wametengana (Kata isiyotakiwa)
13. Taja majina ya watu watatu (3) wasiozidi watatu ambao wataruhusiwa kumtembea mwanafunzi kila Jumapili ya Mwisho wa mwezi pamoja na picha zao (Passport size) za rangi moja.

**AHADI YA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI:**

Mimi ____________________________________________ambaye ni Mzazi/Mlezi wa _____________________________________kutoka shule ya ____________________ Wilaya ya ____________________________Mkoa wa _________________________ Nimeyasoma na kuyaelewa maagizo ya kujiunga na shule hii na niaahidi kulipa michango na kumpa mahitaji mengine mwanangu aliyetajwa hapo juu, mpaka anamaliza **ELIMU YA SEKONDARI**.

**THE PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

**FROM**
THE HEADMISTRESS,
KITAMA SECONDARY SCHOOL,
P.O. BOX 83
**TANDAHIMBA – MTWARA**
**Date………………………..**

**TO:**
The Medical Officer,
…………………………………………..
……………………………………………
……………………………………………

**Re: NAME**
**…………………………………………………………………………………………………**
**……………………………………………………………………………………………..**
**..........,...............................................................................**
Please Examine the above as to her/his Physical and mental fitness for full time course of secondary Education At Kitama Secondary School.

**MEDICAL CERTIFICATE**
I have examined the above named students and consider that She/He is Physically and mentally fit/Until for a full time course of secondary Education at Nangwanda Secondary school.

1. Eye sight…………………………………………………………………………….......... ...............................
2. Hearing………………………………………………………………………………….. ......................................
3. Speech………………………………………………………………………………….. ......................................
4. Venereal diseases………………………………………………………………….................... ...........…..
5. Neurosis………………………………………………………………………………… ......................................
6. TB……………………………………………………………………………………….... .......................................

7. Pregnancy
………………………………………………………………………………………………...................................

8. Any other health problem
………………………………………………………………………………………………

Doctor Remarks
………………………………………………………………………………………………..................
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………....................................................................................................

Doctor's Name ………………………………………………………………………………….
Signature ……………………………………Rubber stamp………………………………
Date
………………………………………………………………………………………............